**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA / UJIJI**

SHULE YA SEKONDARI KICHANGACHUI
S. L. P. 524,
KIGOMA.
14/12/2020

KUMB. NA KCSS/II/09/2021
MZAZI/MLEZI WA ______________________________
SHULE YA MSINGI______________________________

YAH **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE.**

Nafurahi kukuarifu kuwa Mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2021, katika SHULE YA SEKONDARI KICHANGACHUI. Mhula wa kwanza wa masomo utaanza **tarehe 11/01/2021**. Siku ya jumatatu saa 1:30 asubuhi. Kwa hiyo anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na **mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/01/2021**. Siku hiyohiyo masomo yataanza, hivyo **kuwahi ni Muhimu**. Wakati wa kuripoti aje na vitu vifuatavyo:-

**SARE YA SHULE.**

(a) WAVULANA.

(i) Suruali mbili (02),kitambaa aina ya "**DAMU YA MZEE**" iwe na linda za mbele na mifuko mitatu . Asishone ya kubana miguu (model), wala isiyokubali kupanda kiunoni.
(ii) Shati mbili (02) nyeupe zenye mikono mifupi zisizo na marembo yoyote.
(iii) Mkanda mweusi wenye chuma kidogo kisicho na marembo yoyote.
(iv) Tai ndefu inayofanana na kitambaa cha suruali.

(b)WASICHANA.

**(i)** Sketi mbili (02) kitambaa aina ya "**LIGHT GREEN**" zenye malinda ya kupanda, **zivuke magoti (za kufunika soksi za viatu) na wala zisibane mwili.**
**(ii)** Shati mbili (02) nyeupe zenye mikono mifupi zisizo na **marembo yoyote**
**(iii)** Wanaopenda kuvaa Hijabu, wanatakiwa kushona hijabu ndefu inayofunika mikono, rangi nyeupe, isiwe na malesi,wala **marembo yoyote**

(c ) KWA WANAFUNZI WOTE.

(i) Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na visivyo na kisigino kirefu, jozi mbili (02) pamoja na soksi nyeupe.
(ii) Sare ya michezo kwa wavulana ni fulana ya Orange, bukta ya blue na raba; wasichana vivyo hivyo isipokuwa wao wanaongeza sketi ya light blue.
***(iii) Mwanafunzi anatakiwa kuwa amechomekea shati lake na kufunga tai muda wote.***

NB.**SARE ILIYOKOSEWA MSHONO HAITAKUBALIWA SHULENI.**

**2.VIFAA VYA TAALUMA.**

Unashauriwa kumnunulia mwanao vifaa vifuatavyo:-

I. Dictionary ya Kiingereza kwa Kiingereza
II. Mkebe wa mahesabu (mathematical set)
III. Daftari kubwa size 12A au zaidi zisizo pungua 11.
IV. Begi ndogo la kubebea daftari.
V. Kalamu za bluu au nyeusi za kutosha, penseli, kifutio cha penseli na rula.

NB: Mzazi unaweza kumnunulia mwanao vitabu vya kiingereza kama msingi mkuu wa kujifunza masomo mengine; kwa kuwa ni lugha ya kujifunzia. Baadhi ya vitabu hivyo ni:-

a) Mabala the farmer
b) Hawa the Bus driver
c) Kalulu the Hare
d) Fast money
e) Magic garden

**MAAGIZO MENGNE.**

- Mwanafunzi aje na cheti halisi cha kuzaliwa (Original) na nakala ya cheti hicho.
- Mwanafunzi aje na picha mbili za passport size, zilizopigwa kwenye kitambaa cha bluu.
- Soma kwa makini maelezo yote, sheria za shule na kisha ujaze form zilizoambatishwa, Ukurasa wa 4 na 5, na utakuja nazo shuleni.
- Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba, 0754523125

**HONGERA NA KARIBU SANA KICHANGACHUI SEKONDARI.**

..............................

**FABIAN M. KIPECHE**
**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
KICHANGACHUI SEC.SCHOOL
KIGOMA

**OFISI YA RAIS TAMISEMI, MANISPAA YA KIGOMA UJIJI**
**SHULE YA SEKONDARI KICHANGACHUI**
**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 na miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu. Kwa hiyo kila mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa / analazimika kuzifuata sheria na kanuni za shule kama zifuatavyo:-

1. Kuwa na heshima kwa walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla. Hili ni jambo la lazima, kwa hiyo kukosa heshima ni utovu wa nidhamu.
2. Kuwa na mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule, kulingana na ratiba ya shule ni lazima. Mf. Kuingia darasani kuandika na kufanya mazoezi aliyopewa na walimu. Kutokufanya mazoezi au mtihani ni kosa. Kimsingi utoro wowote ni kosa.
3. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni.
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa shuleni.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii. Kutoka ndani ya mipaka bila ruhusa ni kosa.
6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa na sheria ya shule. Ni makosa kuvaa heleni, pete, bangili, mikufu n.k. Tena ni makosa kuvaa sare bila nidhamu. Mfano:- Kutochomekea shati au fulana, kudebedesha suruali, kukunja suruali n.k.
8. Ni marufuku kutinda nyusi, kusuka nywele, kufuga ndevu, kucha, nywele ndefu, kunyoa panki au kipara.
9. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote. Kuchelewa au kutokuzingatia ratiba ni kosa.
10. Kutunza mali za umma. Kuharibu mali yoyote ya umma au shule ni kosa.
11. Hairuhusiwi mwanafunzi kutumia pombe au kileo chochote ndani au nje ya shule. Aidha hairuhusiwi kufika au kukaa kwenye kilabu, baa ya pombe, nyumba ya kulala wageni na kumbi za starehe bila sababu maalum na ya msingi.
12. Hairuhusiwi mwanafunzi; kusema uongo, kudhihaki / kutukana walimu au viranja, kukwepa kazi za mikono, kubishana na walimu ,walezi au viranja. Kama haujaridhika na maamuzi ya mwalimu au kiranja dhidi yako; eleza tatizo lako kwa mwalimu wa zamu, au wa darasa, au mwalimu wa ushauri nasaha, au mwalimu wa malezi na nidhamu. Kama bado haujaridhika nenda kwa makamu mkuu wa shule.
13. Ni makosa kwa mwanafunzi kukaidi wito, unapoitwa na kiranja, mwalimu au walezi.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE MOJA KWA MOJA.**

1. Kuiba au kusaidia tendo la wizi.
2. Kuwa mzinzi au mwasherati au ushoga.
3. Ubakaji au kusaidia tendo la ubakaji.
4. Kupata au kutoa mimba au kusababisha mimba.
5. Ulevi wa pombe, na matumizi ya madawa ya kulevya Mf: uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, sigara n.k.
6. Kupiga wengine au kupigana.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa, au chama chochote cha siasa na picha za viongozi.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kugoma, kuchochea, kusababisha au kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruga amani /usalama wa shule au watu.
11. Kukataa, au kugomea adhabu kwa makusudi.
12. Kuwa na simu ya mkononi.

**UTAWALA**

# HISTORIA YA MWANAFUMZI NA UKOO WAKE

1. *Jina kamili la mwanafunzi*________________________________
2. *Dini /Dhehebu*____________________ *Tarehe ya kuzaliwa*________________
3. *Jina kamili la baba mzazi /ndugu mlezi anyeishi naye*____________________

   *Anuani: Kijiji/Mtaa* ________________________________

   *S. L. P*____________________ *SIMU*____________________

   *Kazi yake*______________________________________

   *Mahali anapofanyia kazi*________________________________

4. *Jina kamili la mama mzazi/Ngugu, Mlezi anayeishi naye*____________________

   ______________________________________________

   *Anuani : Kijiji/Mtaa*________________________________

   *S. L. P* ____________________ *simu* ____________________

   *Kazi yake*______________________________________

   ***Mahali anapofanya kazi***________________________________

5. ***Habari za jamaa na familia ( Ukoo) Wanaoweza kukusaidia wakati wa matatizo***

| S/N | JINA | UMRI | UHUSIANO | KAZI YAKE | ANUANI | SIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |

### JIOGRAFIA YA MAKAZI

1) ***Jina la mtaa unayoishi***________________________________
2) *Barabara ya* ________________________________
3) *Namba ya nyumba unayoishi*________________________________
4) *Jina la Kata unayoishi*________________________________

### KIAPO CHA KUKUBALI/KUTOKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

*Mimi* ____________________*.Ninakubali/sikubali kujiunga na shule hii kwa sababu*________________________________________

______________________________________________

*Sahihi ya mwanafunzi*____________________ *Tarehe*____________________

***THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA***

***MINISTRY OF EDUCATION AND VOCTION TRAINING***

***FORM FOR MEDICAL EXAMINATION***

***To be completed by a medical officer of Government Hospital/ Health Center in respect of all form one entrant.***

***Pupils' Full name*** ____________________________________________

***Age*** ______________________________ ***Year of birth*** __________ ***Sex*** ______

***Blood found (Red and White)*** ____________________________________________

***Stool examinations*** ____________________________________________

***Urinalysis*** ____________________________________________

***Syphilis and other venereal Diseases Test*** ______________________________

____________________________________________

***T. B Test*** ____________________________________________

***Eye Test*** ____________________________________________

***Ears*** ____________________________________________

***Chest*** ____________________________________________

***Spleen*** ____________________________________________

***Abdomen*** ____________________________________________

***Urine Pregnancy Test*** ____________________________________________

***Additional information (If any Eg:- Physical defects impairment (s) (Eg: arm, leg) infection chronic or families disease etc).***

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

***I certify that the above is fit / not fit to pursue further education as stated above.***

***Signature*** ______________________________

***Designation*** ______________________________

***Station*** ______________________________

***Date*** ______________________________ ***Stamp***